**Usitumie mawakala, watakulia pesa yako bure na waweza kukupa cheti cha bandia**

**MUHIMU**

- Kizazi au Kifo kikitokea hospitali au kituo cha Afya HAKIKISHA mhusika haondoki hospitalini au kituo cha Afya bila kupatiwa TANGAZO LA KIZAZI kwa kizazi au KIBALI CHA MAZISHI kwa kifo. Nyaraka hizi ni muhimu katika uandikishaji na hutolewa BURE.
- Kwa kizazi/kifo kilichotokea nyumbani, wasiliana na ofisi ya mtendaji wa kijiji au mtaa ili kupatiwa waraka wowote wa kuthibitisha kutokea kwa Kizazi au Kifo.

**Ni nini faida za uandikishaji Vizazi/ Vifo?**
**VIZAZI**

- Utambulisho wa nasaba ya mhusika
- Kujua umri kwa masuala ya kuanza shule, kustaafu, kinga ya mashtaka ya jinai, kupiga kura, kupata leseni za kuendesha gari, kumiliki silaha n.k
- Kupatiwa hati ya kusafiria (passport)
- Uzuiaji wa ajira za watoto, utumiaji watoto katika vita.
- Kuwezesha serikali kujua idadi ya watu kwa mipango ya maendeleo.
- Kuiwezesha Serikali kujua '*fertility rate*' ya mahali.
- Hatua mojawapo ya kuthibitisha uraia wa mhusika.
- Ni haki ya mtoto kupata cheti cha kuzaliwa (Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto).

**VIFO**

- Kuwezesha ufunguaji mirathi na kudai haki za marehemu; kama bima, benki n.k.
- Kuondoa shitaka la jinai Mahakamani.
- Kuiwezesha Serikali kujua sababu za vifo kwa watu na kutafuta suluhishi.
- Kuwezesha vizuka kupata misaada.

**Nani anawajibika kuandikisha?**

- Wajibu wa kuandikisha kizazi ni wa wazazi kama wazazi hawapo, walezi, mkunga aliyeshuhudia.
- Wajibu wa kuandikisha kifo ni wa jamaa wa marehemu ambaye kifo kimetokea akiwepo au amepata taarifa zake au daktari aliyemhudumia marehemu

**ANGALIZO**
Ni kosa la jinai chini ya Sheria ya uandikisaji vizazi na vifo kwa kushindwa au kuzembea kuandikisha kizazi au kifo, au kutoa taarifa za uongo mbele ya msajili wa vizazi na vifo kwa nia ya kujipatia cheti cha kuzaliwa au kifo.

**ADA**
**Ada zinazotozwa kwa vyeti**
1. Kizazi kilichoandikishwa ndani ya siku 90 - **TSh 3,500/=**
2. Kizazi au kifo kilichoandikishwa zaidi ya siku 90 lakini chini ya miaka 10 **Shs 4,000/=**
3. Kizazi au kifo kilichoandikishwa zaidi ya miaka 10 **TSh 10,000/=**
4. Kifo kilichoandikishwa ndani ya siku 30 **TShs 3,500/=**
5. Kifo kilichoandikishwa zaidi ya siku 30 **TShs 4,000/=**
6. Kupatiwa nakala ya cheti cha kizazi au kifo badala ya Cheti cha awali **Ths 3,500/=**

**NB** - Ada hizi zinaweza kubadilika wakati wowote
- Ada 1-5 ni kwa uandikishaji na utoaji wa cheti mara ya kwanza.

**NDOA NA TALAKA**
Ndoa na Talaka zinatawaliwa na Sheria ya Ndoa ya (Sura ya 29 toleo la 2002).

**Mfungishaji Ndoa (Msajili wa Ndoa)**

- Ndoa hufungwa mbele ya Msajili wa Ndoa (Padre, Sheikh, Mchungaji n.k.) aliye na leseni iliyotolewa na Msajili Mkuu wa Ndoa
- Wafungishaji wa Ndoa za Kiserikali (Mkuu wa Wilaya au Katibu Tawala wa Wilaya) hawahitajiwi kuwa na leseni.
- Mfungishaji wa ndoa anawajibika baada ya kufungisha ndoa kusajili ndoa hiyo na kutoa cheti cha ndoa na kutuma nakala ya ndoa zilizofungwa kila mwisho wa mwezi kwa RITA

**TALAKA**
Mamlaka ya kuvunja ndoa na kutoa talaka ni ya Mahakama. Ndoa ikishavunjwa, Mahakama inatakiwa kumtumia Msajili Mkuu wa Ndoa nakala ya amri (decree) ili aweze kuisajili na kufuta ndoa iliyovunjwa kwenye daftari la ndoa.

**WASILIANA NA RITA KUPITIA ANUANI IFUATAYO:**

**MAKAO YA MUDA**
Afisa Mtendaji Mkuu
Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini
Mtaa Kipalapala Kiwanja Na. 516
Upanga

Wakala wa Usajili,Ufilisi na Udhamini
Kwa Wilaya yoyote Tanzania Bara.

Au waweza kutembelea tovuti yetu **www.rita.go.tz**

**RITA KWA ULINZI WA HAKI YAKO YA KISHERIA**

# IJUE RITA

## REGISTRATION INSOLVENCY AND TRUSTEESHIP AGENCY

## WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI (RITA)

### RITA ni nini?

RITA ni Wakala wa Serikali chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria. Wakala huu umeundwa kutoka iliyokuwa Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu, ambayo hujulikana sana kama Vizazi na Vifo, Msajili Mkuu wa Ndoa na Talaka au Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu. Maneno haya yote huelezea Ofisi ambayo kwa sasa imebadilishwa na kuwa Wakala kutoka Idara ya Serikali. Kazi zilizokuwa zikifanywa na Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu, sasa zinafanywa na RITA. Vile vile huduma nyingine zitaongezwa ili kukidhi mahitaji ya jamii.

Huduma chini ya RITA zimeboreshwa na zinaendelea kuboreshwa ili kutoa thamani halisi ya fedha anazotoa mteja (Value for Money).

Wakala huu umeundwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kuzinduliwa rasmi 23 Juni, 2006.

### DIRA

Kuwa chombo chenye ufanisi katika utoaji wa huduma za usajili, ufilisi na udhamini nchini.

### DHIMA

Kusimamia haki kwa usimamizi wenye ufanisi wa kumbukumbu muhimu za maisha ya binadamu, ufilisi na udhamini ili kuchangia katika maendeleo ya taifa.

unicef

## KAZI ZA RITA:

- Kusimamia Mirathi
- Kusajili Vizazi na Vifo na kutoa Vyeti vya Vizazi na Vifo
- Kutayarisha takwimu za Vizazi na Vifo
- Kutoa Leseni za kufungisha ndoa kwa viongozi wa dini (Mapadre, Wachungaji, Masheikhs n.k.)
- Kutoa vibali maalum vya kufunga ndoa bila kutangaza siku 21
- Kutoa vibali kuruhusu ndoa kufungwa mahali maalum (e.g. hotelini, hospitali n.k.)
- Kusajili ndoa na kutoa nakala za Shahada za Ndoa
- Kutoa Shahada ya kutokuwepo pingamizi la ndoa kwa raia wa Tanzania (mkazi wa Tanzania Bara) anayetaka kufunga ndoa nje ya nchi.
- Kusajili na kutoa Hati ya Muunganisho kwa Wadhamini wa Vyama vya Siasa, Vikundi, Makanisa, Miskiti na Mali.
- Kusajili watoto wa kuasili na kutoa Hati za kuasili.
- Kusimamia mali isiyokuwa na mwenyewe au ya watu walio chini ya umri wa utu uzima.
- Kufanya shughuli za ufilisi na upokezi rasmi
- Kusajili makubaliano (Deeds of Arrangements).

## MTANDAO

Licha ya ofisi ya Makao Makuu iliyoko mtaa wa Kipalapala, Dar es Salaam, RITA ina ofisi kila wilaya ya Tanzania Bara. Ofisi za Wilaya ziko katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kila wilaya.

## MATARAJIO

RITA inakusudia kuboresha huduma zake kwa kuweka kumbukumbu zake katika Komputa ili kuongeza ufanisi. Vile vile RITA iko mbioni kuanzisha huduma ya Kuhifadhi Wosia.

## TARATIBU ZA KUPATA HUDUMA ZA RITA

### 1. USIMAMIAJI MIRATHI.

- Kwa jamaa ya marehemu au mtu anayemdai marehemu au mtu yeyote mwenye uchungu (interest) na mirathi ya marehemu kupeleka ombi mahakama yenye mamlaka akiomba mahakama imteue Kabidhi Wasii kuwa msimamizi, na mahakama kufanya uteuzi; au
- Mahakama yenye kusikiliza ombi la kumteua msimamizi kusimamia mirathi yaweza badala ya kumteua mwombaji kumteua Kabidhi Wasii; au
- Jamaa wa marehemu kuleta ombi kwa Kabidhi Wasii kuomba asimamie mirathi ya jamaa yao. Ombi hili laweza kuwasilishwa ama moja kwa moja au kwa kupitia kwa Katibu Tawala wa wilaya zilipo mali za marehemu.
- Kabidhi wasii atasimamia mirathi kwa kulipa madeni ya marehemu, kudai madeni ya marehemu, kutoa matunzo katika kipindi cha mpito na mwisho atawarithisha warithi kuzingatia wosia wa marehemu (kama upo), sheria inayohusika ama makubaliano ya warithi.
- Huduma hii hutozwa ada ndogo ukilinganisha na faida na kazi yenyewe.

### 2) HUDUMA YA UFILISI.

Ufilisi ni utaratibu wa kisheria unaomwezesha mtu au kampuni ambaye/o imefilisika kumalizana na wadeni wake kwa mali zake kuwekwa chini ya usimamizi wa mfilisi atakayeziuza na kulipa madeni yote au sehemu yake kama kiasi kinachopatikana hakitoshi.

- Wakala hutoa huduma za ufilisi wa watu binafsi (bankruptcy) na ufilisi wa makampuni (company liquidation)
- Taratibu za Ufilisi zimeelezwa katika Sheria ya Ufilisi ( sura ya 25 ya Sheria za Tanzania Bara toleo la 2002) na Sheria ya Makampuni( sura ya 212 toleo 2002) pamoja na kanuni zake.
- Mahakama Kuu ndiyo pekee yenye mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ufilisi.
- Mpokezi Rasmi (Official Receiver/Administrator General) akishateuliwa atafuata taratibu kama zinavyoelekeza katika sheria na mwisho kufilisi mali za mfilisiwa na kulipa wadeni wake na kama kuna alibaki anapewa mfilisiwa au wenye hisa.

### 3) MUUNGANISHO WA WADHAMINI.

- Muunganisho wa Wadhamini ni utaratibu unaoviwezesha vikundi, vyama vya siasa, makanisa, misikiti, au watu waliokabidhiwa mali ya dhamana kwa manufaa ya jamii kuandikisha wadhamini wake na kupata hadhi ya utu wa kisheria (legal personality)
- Wadhamini walioteuliwa na chombo husika watawasilisha maombi ya kusajiliwa katika ofisi za Wakala Makao Makuu na kulipia ada ya shs. 100,000/= ( ada ya sasa).
- Msimamizi Mkuu wa Wadhamini (Administrator General) akikubali maombi atatoa hati ya Muunganisho wa Wadhamini.

### 4) UDHAMINI WA MALI ISIYOKUWA NA MWENYE AU WATOTO WALIO CHINI YA UMRI WA MIAKA 18

- Mali yeyote yenye maslahi ya umma endapo inatokea kwamba chombo kilichokuwa kinaishikilia kimetoweka, Mahakama Kuu kwa maombi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali chini ya sheria ya Mdhamini wa Serikali (sura 31 toleo 2002) itamteua mdhamini wa serikali (public trustee) kushikilia mali hiyo mpaka hapo patakapopatikana chombo kingine cha kushika mali hiyo.

Utaratibu huu uliwahi kutumika;-

* Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipovunjika mwaka1977.
* Muungano wa vyama vya ushirika ulipofutwa mwaka 1993.
* OTTU/TFTU ilipofutwa mwaka 2003.

- Kisheria mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 hawezi kurithishwa . Endapo hii inatokea na hakuna jamaa aliye tayari kuwa mlezi "guardian" wa mtoto huyu ili ashikilie hisa zake, basi Mdhamini wa Serikali huweza kukabidhiwa hisa za mtoto na Msimamizi wa Mirathi (Kabidhi Wasii) mpaka hapo mtoto atakapofikisha umri wa utu uzima na kukabidhiwa hisa zake.

### 5) USAJILI WA VIZAZI, VIFO, NDOA NA TALAKA.

**Taratibu za Uandikishaji Kizazi au Kifo**

(i) Kizazi kinatakiwa kuandikishwa ndani ya muda wa siku 90 na kifo ndani ya siku 30. Kizazi kikiandikishwa ndani ya muda huu wa siku 90 uandikishaji huwa ni BURE isipokuwa mhusika atalazimika kulipa endapo anataka kupatiwa cheti cha Kizazi au Kifo.

(ii) Kizazi au Kifo kilichochelewa kuandikishwa ndani ya muda ulioelezwa kwenye (i) hapo juu, kitaandikishwa baada ya kujaza fomu na kulipa ada ya kushughulikia ombi.

- *Kama kizazi kimechelewa zaidi ya siku 90 lakini chini ya miaka 10 , jaza Fomu BD 15; na kama ni zaidi ya miaka 10, jaza fomu BD 15 A.*
- *Kifo kilichochelewa kuandikishwa baada ya siku 30, jaza fomu BD6.*

**NB:** Fomu hizi hutakiwa kuambatanishwa nyaraka mbalimbali na viapo kuthibitishwa kutokea kwa kizazi au kifo kinachoombewa kuandikisha. Fomu hizi zinapatikana ofisi za Wakala ya Wilaya kwa kila Wilaya na **haziuzwi**. Vilevilewaweza kuzipata katika tovuti ya RITA

**Wapi tukaandikishe Vizazi/Vifo?**

Kifo au Kizazi kitaandikishwa katika daftari la Kizazi au Kifo la Wilaya kilipotokea. Ni marufuku kuandikisha Kizazi au Kifo katika daftari la wilaya ambapo hakikutokea.

Kizazi au kifo kikitokea hospitali au kituo cha afya ni lazima kiandikishwe hapo hapo kilipotokea ndani ya siku 90 kwa kizazi na siku 30 kwa kifo. Endapo muda huu utakuwa umepita kabla ya kuandikisha, basi wahusika wawasilian na Msajili wa wilaya aliyeko katika ofisi za wakala wilayani kwa kuandikisha.

Vizazi vilivyotokea majumbani viandikishwe kwa viongozi wa kijiji, Afisa Tarafa kama huduma ya Usajili inatolewa, na kama haitolewi viandikishwe kwa msajili wa wilaya.